

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



MKUTANO WA NANE

YATOKANAYO NA KIKAO CHA TATU

7 SEPTEMBER, 2017

MKUTANO WA NANE
KIKAO CHA TATU TAREHE 7 SEPTEMBER, 2017

I. DUA:

Naibu Spika (Mhe. Tulia Ackson) Alisoma Dua na kuongoza Kikao cha Bunge.

Makatibu Mezani:

1. Ndg. Charles Mloka
2. Ndg. Neema Msangi

II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

1. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira na Muungano), Mhe. January Yussuf Makamba aliwasilisha:-

Taarifa ya Mwaka na Hesabu zilizokaguliwa za Baraza la Taifa la Hifadhi ya Mazingira (NEMC) kwa Mwaka wa Fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2016 (*The Annual Report and Audited Accounts of National Environment Management Council (NEMC) for the Year ended 30th June, 2016*).

2. Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji, Mhe. Isack Aloyce Kamwelwe aliwasilisha:-

Azimio la Bunge la Kuridhia Mkataba wa Uanzishwaji wa Kamisheni ya pamoja ya Bonde la Mto Songwe kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Jamhuri ya Malawi (*Convention on the Establishment of a Joint Songwe River Basin Commission between the Government of the United Republic of Tanzania and the Government of the Republic of Malawi*).

3. Mjumbe wa Kamati kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji, Mhe. Salum Mwinyi Rehani aliwasilisha Mezani:-

Maoni ya Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji juu ya Azimio la Bunge la Kuridhia Mkataba wa Uanzishwaji wa Kamisheni ya Pamoja ya Bonde la Mto Songwe kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Jamhuri ya Malawi (*Convention on the Establishment of a Joint Songwe River Basin Commission between the Government of the United Republic of Tanzania and the Government of the Republic of Malawi*).

4. Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani kwa Wizara ya Maji na Umwagiliaji, Mhe. Hamidu Hassan Bobali aliwasilisha Mezani:-

Maoni ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani juu ya Wizara ya Maji na Umwagiliaji kuhusu Azimio la Bunge la Kuridhia Mkataba wa Uanzishwaji wa Kamisheni ya Pamoja ya Bonde la Mto Songwe kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Jamhuri ya Malawi (*Convention on the Establishment of a Joint Songwe River Basin Commission Between the Government of the United Republic of Tanzania and the Government of the Republic of Malawi*).

5. Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi (kwa niaba ya Mhe. Selemani Said Jafo, Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI) aliwailisha Mezani:-

Azimio la Bunge la Kuridhia Itifaki ya Amani na Usalama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (*The East African Community Protocol on Peace and Security*).

6. Mhe. Rose Cyprian Tweve (kny: Mwenyekiti wa Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama:

Maoni ya Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama juu ya Azimio la Bunge la Kuridhia Itifaki ya Amani na Usalama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (*The East African Community Protocol on Peace and Security*).

7. Msemaji wa Kambi ya Upinzani Kuhusu Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mhe. Masoud Abdallah Salim aliwasilisha Mezani:-

Maoni ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani juu ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kuhusu Azimio la Bunge la Kuridhia Itifaki ya Amani na Usalama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (*The East African Community Protocol on Peace and Security*).

III. MASWALI:

Maswali yafuatayo yaliulizwa na Waheshimiwa Wabunge:-

OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

Swali Na. 30. Mhe. Bupe Nelson Mwakang'ata

Nyongeza: Mhe. Bupe Nelson Mwakang'ata
Mhe. Omary Ahmed Badwell
Mhe. Aida Joseph Khenan
Mhe. Halima Abdallah Bulembo

Swali Na. 31. Mhe. Joseph Roman Selasini (kny: Mhe. James Francis Mbatia)

Nyongeza: Mhe. Joseph Roman Selasini

OFISI YA RAIS (UTUMISHI NA UTAWALA BORA):

Swali Na. 32: Mhe. Mahmoud Hassan Mgimwa (kny: Mhe. Cosato David Chumi)

Nyongeza: Mhe. Mahmoud Hassan Mgimwa
Mhe. Nuru Awadh Bafadhili
Mhe. Innocent Lugha Bashungwa

WIZARA YA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:

Swali Na. 33: Mhe. Neema William Mgya

Nyongeza: Mhe. Neema William Mgya
Mhe. Khadija Nassir Ali

WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:

Swali Na. 34: Mhe. Jumaa Hamidu Aweso

Nyongeza: Mhe. Jumaa Hamidu Aweso
Mhe. Hussein Nassor Amar
Mhe. Jerome Dismas Bwanausi
Mhe. Rhoda Edward Kunchela

Swali Na. 35: Mhe. Omar Abdallah Kigoda

Nyongeza: Mhe. Omar Abdallah Kigoda
Mhe. Stanslaus Shing'oma Mabula
Mhe. Hussein Mohamed Bashe

WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO:

Swali Na. 36: Mhe. Masoud Abdallah Salim

Nyongeza: Mhe. Masoud Abdallah Salim
Mhe. Esther Nicholas Matiko
Mhe. Hawa Mchafu Chakoma

WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:

Swali Na. 37: Mhe. Joyce Bitta Sokombi

Nyongeza: Mhe. Joyce Bitta Sokombi
Mhe. Qulwi Willy Qamballo
Mhe. Raphael Masunga Chegeni

WIZARA YA MAJI NA UMWAGILIAJI:

Swali na. 38: Mhe. Josephat Sinkamba Kandege

Nyongeza: Mhe. Josephat Sinkamba Kandege
Mhe. Dunstan Luka Kitandula
Mhe. Maulid Abdallah Mtolea
Mhe. Venance Muthusalah Mwamoto

IV. MATANGAZO:

A: WAGENI

1. JUKWAA LA SPIKA

- (i) Wageni 5 wa Mhe. Mwigulu Lameck Nchemba, Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi ambao ni Viongozi wa Idara na Taasisi za Wizara hiyo wakiongozwa na Katibu Mkuu Meja Jenerali (Mstaafu) Projest Rwegasira.

2. WALIOTEMBELEA BUNGE – MAFUNZO

- (ii) Wanafunzi 45 na Walimu 5 kutoka Shule ya Sekondari Kihesa iliyoko Mkoa wa Iringa wakiongozwa na Mwl. Pius Mwachuvaka.
- (iii) Vijana 60 kutoka Kanisa la Redeemed Assemblies of God (T) la Mkoa wa Dodoma.

B: KAZI

Naibu Spika aliwatangazia Waheshimiwa Wabunge kuwa Waziri Mkuu hayuko Bungeni na nafasi yake amekaimilishwa kwa Mhe. Waziri wa Maliasili na Utalii Mhe. Jumanne Abdallah Maghembe.

MWONGOZO WA SPIKA:

Mhe. Tundu Antiphas Lissu alisimama kwa Kanuni ya 68(7) kuomba Mwongozo kuhusiana na Kanuni ya 120(1) (2) na (3); Kanuni ya 122(1), (2) na (3) na Kanuni 122(4).

Mhe. Tundu Anthiphas Lissu aliomba Mwongozo wa Spika kwamba ni Kanuni gani ya Kibunge iliyotumika kuwasilisha Taarifa za Kamati Maalum ziwasilishwe kwa Waziri Mkuu na siyo Bunge? Na kwamba, kwa kuwa Kamati Maalum ziliundwa kwa Kanuni za Bunge 120(1), (2) na (3) na 122(1), (2) na (3). Taarifa hizo zilipaswa kuwasilishwa ndani ya Bunge na kujadiliwa Kikanuni.

- Je, ni lini Taarifa hizo zitawasilishwa Bungeni ili zijadiliwe Kikanuni?

NAIBU SPIKA

Alijibu kwamba, kwanza jambo lililoombewa Mwongozo halikutokea Bungeni.

Pili, kwa Mujibu wa Kanuni ya 120(1) katika Bunge hili hakuna hoja iliyotolewa mahali kwamba sasa inaundwa Kamati ya Bunge, ni Spika tu amechagua utaratibu wake kwa Kamati alizounda mwenyewe.

Vilevile, Kanuni ya 117(17) inampa Spika uwezo wa kuiambia Serikali juu ya Kamati mahususi alizounda.

V. HOJA ZA SERIKALI:

MAAZIMIO:

1. Waziri wa Maji na Umwagiliaji aliwasilisha Azimio la Bunge la Kuridhia Mkataba wa Uanzishwaji wa Kamisheni ya Pamoja ya Bonde la Mto Songwe kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Jamhuri ya Malawi (*Convention on the Establishment of a Joint Songwe River Basin Commission between the Government of the United Republic of Tanzania and the Government of the Republic of Malawi*).
2. Mwenyekiti wa Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji, Mhe. Christine Gabriel Ishengoma aliwasilisha Maoni ya Kamati hiyo kuhusu Azimio hilo.
3. Msemaji wa Kambi ya Upinzani Bungeni Mhe. Hamidu Hassan Bobali aliwasilisha Maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu Azimio hilo.
4. Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi aliwasilisha Azimio la Bunge la Kuridhia Itifaki ya Amani na Usalama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (*The East African Community Protocol on Peace and Security*).
5. Mwenyekiti wa Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama Mhe. Stephen Julius Masele aliwasilisha Maoni ya Kamati kuhusu Azimio hilo.
6. Msemaji wa Kambi ya Upinzani Bungeni kwa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mhe. Cecilia Daniel Paresso aliwasilisha Maoni ya Kambi kuhusu Azimio hilo.

- | | | |
|-------------------------------|---|---------|
| 1. Mhe. Tundu Antiphas Lissu | - | CHADEMA |
| 2. Mhe. Masoud Abdallah Salim | - | CUF |
| 3. Mhe. Janeth Zebedayo Mbene | - | CCM |
| 4. Mhe. Richard Phillip Mbogo | - | CCM |
| 5. Mhe. Moshi Selemeni Kakoso | - | CCM |
| 6. Mhe. Marwa Ryoba Chacha | - | CHADEMA |

VI. KUSITISHA BUNGE

Saa 7:00 mchana Bunge lilisitishwa mpaka saa 11:00 jioni.

VII. BUNGE KUREJEA

Waheshimiwa Wabunge waliendelea kuchangia Maazimio, ikiwa ni baada ya TAARIFA YA SPIKA kuhusu tukio lililompata Mhe. Tundu Antiphas Lissu la kupigwa risasi na kwamba anaendelea kupatiwa matibabu.

- | | | |
|---|---|-----|
| 7. Mhe. Rashid Abdallah Shangazi | - | CCM |
| 8. Mhe. Oran Manase Njeza | - | CCM |
| 9. Mhe. Esther Michael Mmasi | - | CCM |
| 10. Mhe. Salum Mwinyi Rehani | - | CCM |
| 11. Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi, Mhe. William Tate Olenasha | | |
| 12. Waziri wa Habari, Sanaa na Michezo, Mhe. Harisson George Mwakyembe | | |
| 13. Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji, Mhe. Eng. Isack Aloyce Kamwele | | |

Hoja ya Azimio la Bunge la Kuridhia Mkataba wa Uanzishwaji wa Kamisheni ya Pamoja ya Bonde la Mto Songwe kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Jamhuri ya Malawi liliridhiwa na Bunge.

- | | | |
|--|--|--|
| 14. Naibu Waziri wa Mambo ya Nje – Mhe. Suzan Alphonse Kolimba | | |
| 15. Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi – Mwigulu Lameck Nchemba | | |

Hoja ya Azimio la Bunge kuhusu Itifaki ya Amani na Usalama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki liliridhiwa na Bunge.

Naibu Spika alikumbusha matumizi ya Kanuni 154.

VIII. KUAHIRISHA BUNGE

Saa 12:10 jioni Bunge liliahirishwa hadi Alhamisi tarehe 8 Septemba, 2017 saa 3:00 Asubuhi.